Kazi: Mdudu Mbaya Zaidi

Florence Chanya Mwaita

"Akikuuma lala, upige usiahi," ndivyo wasemavyo wataalamu kuhusu mdudu mmoja wa nchi kavu kwani mwathiriwa hupatwa na uchungu usiomithilika.

Katika historia ya wadudu, ni huyo tu ambaye kutajwa kwake hunitia mahoka. Sio kwa sababu ya miguu yake mirefu au mabawa yake ya rangi ya kutu. Hata mwiba wake wenye sumu yenye uwezo wa kulemaza haunitishii maisha, kwani ni muhali sana kumuua binadamu.

Jambo linalonitishia maisha zaidi kuhusu nyigu kupe wa aina ya tarantula, ni hila zake za kumwinda buibui hatari aitwaye tarantula. Sio kwa ajili ya kujitafutia mlo, kwani nyigu huyo hula matunda au uki wa maua, isipokuwa, ni tabia yake ya kulamzimisha buibui kuwa mwenyeji wa watakapozaliwa wanawe.

Toba, masikini roho yangu ndogo! Kufikia sasa, siwezi kutazama video za vita vya nyigu kupe dhidi ya buibui, kwenye mtandao wa Youtube, bila kuishikilia. Naogopa ajabu.

Aisee sitii chumvi, nyigu kupe humwandama buibui bila huruma, humvamia akamchoma kwa mwiba wake wenye sumu inayolemaza. Akilegea tu nyigu humpara mgongoni akataga yai lake ndanimwe kisha humburura hadi mafichoni, anapomuacha baada ya kuziba tundu alilopekecha. Ikumbukwe kuwa buibui wa aina ya tarantula ni mkubwa zaidi ya nyigu na ni mzito sana ikilinganishwa na kidudu kinachomtendea unyama huo. Hali kadhalika, buibui mwenyewe ni hatari; lakini ataachwa hoi, hajui kilichomkuta, hana tofauti na aliyekufa, na kifo chake ni taratibu na kichungu zaidi.

Kwa kuwa nyigu wa aina ya tarantula ni vimelea, yai lililotagwa ndani ya buibui litaangua kiwavi kitakachorutubishwa na mwili wa buibui aliyeathirika, kabla ya kugeuka buu, na hatimaye mdudu kamili. Yaani yule buibui ataliwa ndani kwa ndani na kiwavi wa nyigu. Akiwa hai! Kwa wiki kadhaa! Sijui wajuavyo viwavi hao, kuwa inawapaswa waanze na viungo visivyo hatari kwa usalama wa buibui, ili wasimuue mara moja, wabaki bila chakula, au makao!

Ninachojua ni kuwa, kiwavi kitageuka buu, kikisitiriwa na buibui huyo, na buu litakapokuwa mdudu kamili, mwenyeji wake hatakuwa zaidi ya kaka tupu la yai. Kajifia kitambo, akimwachia nyigu fursa nyingine ya kuendelea na mzunguko wa maisha yake!

Wakati wote huo, buibui hana uwezo wa kuzuia kinachomjia. Kinga yake ya mwili haiwezi kuliharibu yai geni ndani ya mwili wake. Nyigu huachia kemikali zinazozuia kinga ya buibui kudhuru kizazi chake. Ikiwa sauti zozote zitasikika kutoka kwenye "kaburi" anamoachwa buibui, sio za kiwavi anayefurahia mlo wake. Ni za kite cha buibui anayeliwa ndani kwa ndani akiwa hai.

Keti kitako sasa nikwambie: Hatari alivyo nyigu huyu; nyigu huyu na ubaya wake huo; hashindi mdudu mmoja mwenye miguu miwili, avaaye nguo badala ya mabawa; anayetembea badala ya kuruka au kupuruka; mwenye akili inayopaswa kuwa timamu na katu sio razini. Nyigu muuaji ni mdudu mbaya. Lakini mwanasiasa mbinafsi ni mdudu mbaya zaidi.

Vituko vyote hivyo vya nyigu mkubwa zaidi duniani – takriban sentimita kumi – ni mnyama mwoga zaidi. Mwanzo huishi peke yake. Na si rahisi kumdhuru binadamu au mnyama yeyote yule. Labda awe hatarini. Isitoshe hata anapotaga yai lake, ni moja tu. Hatagi mayai mengi ndani ya mwili wa buibui. Cha muhimu zaidi, ningependa utambue kuwa nyigu hufanya hivi kwa sababu ndiyo maumbile. Hachagui mwenyewe kujikuta katika hali hiyo. Ni sheria ya mwitu!

Kwa upande mwingine, mtu anapoitwa mwanasiasa, na anapokuwa na sifa ya ubinafsi, woga humuondoka kabisa kwenye nafsi yake. Ni kama anakuwa na moyo wa chuma. Bali na kung'olewa jino, Adolf Hitler, dikteta wa Kinazi aliyetawala Ujerumani, na kukochea vita vya pili vya dunia, aliogopa nini? Pol Pot, dikteta aliyetawala Kambodia na kusababisha mauaji ya halaiki alimwogopa nani? Nauliza niambiwe, Rais wa tatu wa Uganda, Idd Amin Dada, alipotaka zaidi madaraka, ni kipi kilichomshitua? Ni kipi kilichomsitisha hatua?

Rejelea historia uone jinsi watu wengi walivyopoteza maisha nduli hao walipokuwa madarakani. Na asiniambie mtu kuwa walizaliwa na roho mbaya! Nashadidia kuwa nyigu kupe hana la kufanya, anafuata maumbile na sheria ya mwitu. Katili watatu niliotaja, waliotawala kwa mabavu, na kuchinja binadamu wenzao bila huruma, walikuwa wakifuata sheria gani ya mwitu? Kuna yeyote aliyetetemeka kwa woga baada ya kutoa amri ya watu kuzikwa wakiwa hai? Hamna! Nduli na mchimba dawa shauri lao moja tu.

Elimu yote niliyo nayo, kuhusu nyigu hao vimelea, nasisitiza kuwa hamna anayetaga yai zaidi ya moja ndani ya buibui. Hasemi ati huenda mwanangu mmoja akafa, wengine wakabaki duniani, kuendeleza kizazi changu. Hebu mpe nafasi kidogo mwanasiasa anayejali maslahi yake tu. Atajillimbikizia mali ajabu, na kuhakikisha vizazi vyake vijavyo havijui bei ya mkate.

Nani asiyemjua Marehemu Mobutu Sese Seko, Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, iliyoitwa Zaire? Asiyejua bado hajazaliwa! Sifa zake zilienea kama moto kwenye msitu wa majani makavu. Alikuwa na pesa au pesa – zote za umma. Akajenga majumba ya kifahari, usiseme kasri lenye vioo ambavyo risasi haiwezi kupenya. Kasri ambalo miaka mingi baada ya kifo chake lilikuja kumilikiwa na vipanya na vipopo. Lakini yeye shida haikumjua jina, nadhani ndege alizosafiria zingemuita aitike. Lakini yeye na wenzake wenye hadhi walipenda kuitwa maboga makubwa. Maboga madogo yalilia usiku kwa kwikwi, kwa kukosa chakula cha watoto wao. Maboga madogo yalitamani kuihama nchi yao, yaende yanakothaminiwa. Maboga madogo yakishindwa kuvumilia kuzorota kwa uchumi, maboga makubwa yaliandaa karamu ya kukata na shoka. Kufikia sasa, sijasikia nyigu anayeandaa karamu ya kusherehekea kifo cha buibui.

Unawajua wanasiasa wangapi ambao hawapendi kubanduka madarakani? Afrika pekee imesheheni takriban nusu ya wanasiasa duniani wanaotaka kutawala milele. Vyeo waliumbiwa wao. Vizazi vinavyowafuata visiwe na haraka! Vinaenda wapi na hakuna nafasi? Yaani viongozi wabinafsi ajabu. Utasikia miaka thelathini mtu anatawala, heri kifo kimtenganishe na uongozi. Nao uongozi gani na ni dhuluma tupu. Poh! Hata nyigu mwenyewe hana maisha. Miezi kadhaa anawaachia wengine waendelee.

Ni faraja kubwa kujua kuwa nyigu hana uwezo wa kuzungumza. Mdudu mbaya zaidi amezindua mbinu mwafaka ya kuzidanganya nafsi za watu. Hahitaji kuwa na shahada ya uzamifu au uzamili katika masuala ya siasa, lakini ana tajriba ya kunyenya na kunyenga—yaani kubembeleza kwa maneno yaliyosingwa asali. Hutoa ahadi kubwa kubwa asizoweza kutimiza. Maneno yasipofua

dafu, hutafuta vijizawadi ovyo, na kuwarushia wananchi wa kawaida makombo. Wasiojua kuwa huo ni mtego hunaswa na kukwama pale. Wakizinduka wamekwishamrejesha mdudu mbaya zaidi mamlakani. Anawafyonza damu. Wakilalamika anawabeza:

“Mlinichagua wenyewe, sasa mwatakani?”

“Wajinga ndio waliwao!”

Ataendelea vivyo hivyo, na hatachelea kubadilisha sheria ikiwa itampendelea yeye. Atasahau kabisa sera alizouza wakati wa kampeni. Atakapokuwa akijadili miswada bungeni, inayoruhusu matumizi ya fedha nyingi za umma kuliko serikali inazopata kwa ushuru, utatamani afunge domo. Anyamaze kabisa kama nyigu.

Rangi ya mdudu mbaya inavutia mno ambapo ni njia ya maumbile ya kutahadharisha asidi:

“Kaeni kando, mimi ni hatari kwa usalama wenu!”

“Ni kweli ni maridadi, lakini sio ua la kuchezea.”

“Tahadhari! Vyote ving’aavyo si dhahabu.”

Hivyo wadudu na wanyama au hata watu wapitao karibu na nyigu aina ya tarantula, wana fursa kubwa ya kujilinda kwani watakapomuona mdudu huyu watamwepuka maadamu anaonekana kwa urahisi. Hamna mwanasiasa anayewaonya watu wamwepuke kama mgonjwa wa ukoma. Atahakikisha amekuvizia taratibu, utashtukia huwezi kujitoa kwenye mtego uliokunasa. Kila alifanyalo zuri, fahamu si la bwerere. Utalipia kwa chozi la damu. Akifanya mawili mazuri, kwa hakika matendo kumi yatakuwa yakiondoa wema huo.

Buibui mateka hulemazwa, haendi popote. Anabururwa huku na kule, kuelekea mbali na makao yake. Anafukiwa tunduni. Analazimishwa kuwa mlo na nyumba ya uzazi ya nyigu. Hawezi kuamua atoke mle tunduni apunge upepo! Halishwi. Hanyweshi. Almuradi hana uhuru wowote. Ni mateka. Kinachomjia, kitakachomkuta, hana uhuru wa kukiepuka.

Binadamu aliumbwa akiwa huru. Nyakati zote ambazo amenyimwa uhuru huo mambo yametumbukia nyongo. Kihistoria imemwagika damu nyingi mno binadamu akipigania uhuru wake. Uhuru kutoka kwa mkoloni. Kuuasi ubaguzi wa kikabila na ubaguzi wa rangi na jinsia. Uhuru wa kutangamana na uhuru wa kuzungumza.

Ikiwa mifano hiyo haitoshi, utakumbuka mlipuko wa Virusi vya Korona. Dunia nzima ilifunga mlango ikakaa ndani, isikivuke kizingiti cha mlango. Tulikosa uhuru wa kutoka nje na kutangamana, uhuru wa kuvaa tupendavyo. Ikawa hatuna budi kujisitiri kwa barakoa. Muda si mrefu hayo yalianza kutusinya. Tukachoka kukaa ndani. Nusura wengine wapate kichaa. Walioshindwa wakavunja sheria, waliovumilia ni kwa sababu walijua wanajikinga wenyewe na wawapendao. Na walijua ni kwa muda, lakini kumbuka uchumi ulivyoanza kuzorota.

Tatizo ni kuwa, binadamu anavyotia juhudi apate uhuru, kuna mwingine anayehangaika apate kinyume chake, amyime usingizi. Hii ni kazi ya mdudu mbaya zaidi. Mdudu mbinafsi. Mdudu avaaye suti na kuendesha maswala nyeti ya serikali na umma, kama gari bovu. Mdudu apataye njia na kuhepa mambo yakitumbukiwa nyongo. Akiwaacha nyuma nguruwe. Naam, mkuki kwa nguruwe, kwa binadamu mchungu.

Ukitaka kujua jinsi kukosa uhuru kunavyoweza kuathiri nchi, tembelea Ginekweta, taifa ndogo la Magharibi ya Afrika. Utakumbana na hali ya kukirihi. Nchi iliyobarikiwa na mafuta, lakini wenyeji wake ni wachochole. Wanasiasa wabinafsi wanajilimbikizia mali na kuwanyima wananchi fursa ya kupumua au kushtakia dunia hali yao. Watafanya hivyo kivipi na hakuna uhuru wa vyombo vya habari. Na sio taifa hilo peke yake. Mataifa mengi duniani bado hayana uhuru wa vyombo vya habari. Serikali ndizo zinazomiliki vyombo vyenyewe na hutia kwenye ratili habari zitakazoripotiwa na zitakazofichwa zisijulikane. Haya serikali nyingi hufeli kwa nini? Japo kuna wanasiasa wazuri wanachojua wakifanyacho, hapakosi wadudu wabaya zaidi. Sasa basi inakuwa sio swala lili hili tunalolirejelea. Tayari tumewalemaza, hawawezi kuepuka, lakini ziba mwanya, wasije wakatoroka. Na vilio vyao visiwafikie wengine, acha tu waliwe nyama zao.

Hila hizi za wanasiasa wabinafsi siku zote hunikumbusha wala watu wa Papua Gine, almaarufu kama Wasawi. Ni katika kitabu Peace Child (Mtoto wa Amani), kilichoandikwa na Mmisionari Donald Richardson aliyekwenda huko na mkewe kueneza Injili. Walikumbana na watu "wanaokunenepesha kwa urafiki, wakikutayarisha uchinjwe." Na hawakusita kuhifadhi mafuvu ya vichwa kama medali za ushindi wao. Usione shani basi rafiki yangu, Juda Iskarioti aliyemsaliti Yesu ndiye aliyekuwa shujaa kwao, na sio Mwana wa Mungu, aliyekuja kuikomboa dunia kulingana na Bibilia Takatifu. Heri nyigu wa tarantula. Hamwandalii buibui karamu. Hamchoshi kwa maneno. Hamzubaishi. Buibui anajua kabisa, aniandamaye ni adui. Sio ndugu wa toka ni toke. Sio sahibu.

Sasa tuvirejelee vita vya nyigu na buibui. Wa kwanza, japo mwili wake ni mdogo ukilinganishwa na wa buibui tumwite Goliathi, lile jitu la Wafilisti linalotajwa katika Bibilia. Ana mwili stadi na mwiba wenye sumu kali. Anatarajiwa kabisa kushinda vita. Uongo kando mara nyingi nyigu hushinda. Wa pili tumuite Daudi, aliyepambana na jitu hilo, japo ana mwili mkubwa, uwezo wake ni mdogo sana ikilinganishwa na anayemkabili. Ni muhali sana kwa buibui kuibuka mshindi, lakini nani alisema kuwa haiwezekani? Penye nia pana njia! Buibui akipigana vita vya kufa kupona, kuna uwezekano mkubwa kabisa wa kumdhuru nyigu kiasi cha kumtoa uhai! Nasema hivi: Buibui anaweza kumuua nyigu na kumzuia kuchumkua mateka na kutaga yai ndani yake! Anaweza kumshinda.

Ni jambo la kutia moyo kuwa mdudu mbaya zaidi anaweza kushinda vita vingi, ila sio vyote. Wananchi wakiwa na nia moja, na wamwandame wapigane naye kwa vyovyote vile, tairi yake inaweza kutolewa pumzi. Vitakuwa kama vita vilivyotokea Uhabeshi katika karne ya kumi na tisa; vita vya Adwa. Italia ilidhamiria kuleta ukoloni nchi huru ya Uhabeshi. Ikafika na bunduki na risasi zake, lakini iliambulia patupu dhidi ya Uhabeshi, chini ya uongozi wa Menelik wa Pili. Ndiposa nchi ya Uhabeshi ikaingia katika historia kama nchi ya Afrika ambayo mkoloni alishindwa kupenya. Hadi sasa Uhabeshi inashikilia nafasi hiyo, ikiwa na Liberia – nchi nyingine ya Magharibi mwa Afrika.

Sio kusema kuwa hakuna ukoloni mambo leo. Wadudu wengi wabaya zaidi ni wale waliochukua hatua za uongozi baada ya mkoloni kufunga virago na kwenda zake. Na vizazi vyao vinazidi kuwanyanyasa watu wa mataifa mengi ya dunia. Wadudu hao wabaya zaidi ndio katili zaidi ikilinganishwa na mkoloni. Nyigu hadhuru aila yake. Mdudu mbaya zaidi hajali kama alitoka tumbo moja na anayemwadhibu. Almuradi amekuwa kizingiti cha kupinga akichukua hatamu za uongozi, hatasita kumwangamiza.

Hebu niambieni sasa, kwanini tunawapa upenyo watu kama hao? Kwanini tunawaachia mamlaka na vyeo wasivyostahili tukijua watatukalia mguu wa kausha katika kila jambo. Tukijua kuwa

tutabaki nyuma kiuchumi, kisiasa, kiteknolojia na katika maisha ya kijamii? Kwanini bado hatujafahamu kuwa hawana nia ya kupambana na ufisadi? Na kuwa wafisadi wakubwa ni wao. Wafisadi ambao hawatajali wakituacha sisi tukipigana wenyewe kwa wenyewe, tuking'ang'ania makombo waliyoturushia kama mbwa. Wakati wote huo, mbwa wao wanakula vizuri kutushinda. Haki iko wapi? Waliolala na waamke, vyanda vya miguu havivishwi pete.

Kabla ya kufikia hatua ya kupigana nao, kuna njia inayotumiwa na buibui ambayo tukiitumia vizuri, hawawezi kutufikia. Buibui ana maficho yake, hujijengea utando akajificha humo. Akijenga utando mzuri tu, nyigu hawezi kumfikia humo.

Wakati mwingine nyigu hugusagusa utando wa buibui, kama njia ya hila ya kumhadaa buibui kuwa huenda utandu wake umemnasia chakula. Akitoka tu kuja kuangalia, nyigu huchukua fursa ya kumchoma kwa mwiba wake na kumlemaza. Jambo hili si tofauti na kuku anavyorushiwa mahindi, na kukamatwa akawe kitoweo pindi anapoyafuata. Si tofauti na hila za Wasawi walipokuwa wakitafuta nyama za watu, kwenye vitongoji jirani.

Inaweza kuwa watu hawa hawatuhadai kwa namna ya kugusa maficho yetu. Lakini fuatilia kabisa ujue njia zao:

"Tutawajengea nyumba za wazee!"

"Watoto wenu watasomea ng'ambo!"

"Tutapambana na ufisadi!"

"Tutajenga miundo msingi!"

Ni uongo mtupu! Ndiko kupakwa mafuta kwa mgongo wa chupa huko. Ulimwona wapi mfisadi, mtu asiye na rekodi ya uadilifu, akipambana na ufisadi? Wakisema mambo kama hayo, fikiria haya:

"Tutadaiwa kope si zetu!"

"Tutauziwa hewa!"

"Tutaliwa nyama yetu!"

"Tutalemazwa!"

"Tutafukiwa pangoni!"

"Tutazikwa tukiwa hai!"

Usikubali kura yako iwe sababu ya kuhangaika maisha yako yote. Wewe na vizazi vijavyo. Na najua hapo ndipo penye tatizo. Kwa kiwango kikubwa jamii haina elimu inayostahili kuwa nayo, ya kuipa uwezo wa kufanya uamuzi mzuri. Na wanajua hivyo hawa wabinafsi. Wanajua kuwa wanahitaji tu kufikia wengi wasio na habari ili kupenya. Sasa basi kibarua kinakuwa rahisi kwao; papai kwa kijiko.

Japo tumebaki nyuma mno, haimaanishi tubaki gizani. Tunaweza kujifunza kitu kutoka kwa mataifa yaliyopiga hatua kisiasa, kiuchumi na kwa kila jambo. Tujisaili kwa nini Korea Kaskazini imebaki nyuma kimaendeleo huku Korea Kusini ikipika hatua kila kukicha.

Mbinu ni nyingi. Kwa mfano, vipo vitabu vinavyoweza kujibu maswali tuliyonayo: Kitabu Why Nations Fail (Kwa nini Mataifa Huanguka), cha Profesa Daren Acemoglu, mtaalamu wa maswala ya uchumi, aliyeshirikiana na mwenzake James Robinson, mtaalamu wa uchumi na sayansi ya siasa. Kwa pamoja wanawasikiliza wanasoshiolojia wenye msimamo kuwa mataifa huanguka kwa sababu kama za kijiografia na kitamaduni. Lakini wao wanashikilia kuwa mataifa huanguka kwa sababu za kisiasa.

Kwa kiwango kikubwa hapo pana ukweli kwa kuwa soko huru, miundo msingi, na maisha ya jamii, uhuru wa kutangamana na mifumo ya uongozi hutegemea siasa za nchi. Wanasiasa hawa ndio wanaouza sera, kuunda serikali na kutunga sheria. Ikiwa hazina mwelekeo chanya, basi bila shaka taifa litafeli. Hasa ikiwa siasa za nchi zinaendeshwa na wadudu wabaya zaidi.

Ninaelewa fika kuwa watu wote hawana elimu hii, lakini tunaweza kujitolea kuelimishana. Tukatae zawadi na vitu vya bwerere ambavyo kuvipokea kwetu kunahakikisha tutapata hasara kubwa kesho. Lakini zaidi ya yote, tuwaepuke wadudu wabaya zaidi, watakaotupotosha, na kutupoteza kabisa, ikiwa watatuachia uhai wetu! Kufikia sasa, sijasikia dikteta ambaye hugeuka akawa mwema. Wote hufa wabaya.

Nipo ukingoni sasa na bado nashikilia ki ki ki msimamo wangu. Spishi ya nyigu inayohangaisha buibui ni hatari, lakini ina faida nyingi mno ambazo tutazizungumzia siku nyingine. Mwanasiasa mbinafsi kwa upande mwingine, haina faida yoyote. Ndiposa siogopi kumwita mdudu mbaya zaidi. Ningekuwa kuku, ningekuwa mangisi, manyoya yangu yasimame kwa hasira nimuonapo. Ningekuwa nungunungu, miiba yangu ingekuwa tayari nyakati zote kumshambulia adui yangu huyo. Lakini kwa sasa mimi ni mwandishi, na nadhani nimeutumia wino wangu huu vizuri. Ndiko kukaa ange huku, la sivyo, mdudu mbaya zaidi atahakikisha sina ruhusa ya kuitumia lugha ya Kiswahili katika uandishi! Na hapo sitalemaa tu, atakuwa ameitoa roho yangu.